**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# MUHTASARI WA KISWAHILI UALIMU

## NGAZI YA CHETI

**2009**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# MUHTASARI WA KISWAHILI UALIMU

## NGAZI YA CHETI

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

ISBN.........................................................................................................................

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kunakiliwa, kutafsiriwa, kupigwa chapa au kutolewa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Umebuniwa na Kuandaliwa na:

Taasisi ya Elimu Tanzania,

S.L.P. 35094,

Dar es Salaam

**TANZANIA**

Tel. + 255 – 22 2773005,

Fax: + 255 22 2774420

E-mail: director.tie@tie.go.tz

Website: www.tie.go.tz

**IDHINI**

Kozi ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na imekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye moyo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha darasa la kwanza hadi la saba katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu kozi ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili limeidhinishwa rasmi kuwa ni **Muhtasari wa Kiswahili Ualimu Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009.

**Umeidhinishwa na .......................................................**

**Saini..................................................................................**

**Tarehe...................................................................2009**

**Kamishna wa Elimu**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

S.L.P 9121

**Dar es Salaam**

Simu: +255 222 110150, 110179, 11046

Nukushi: +255 222 113271

Wovuti: www.moe.go.tz

## YALIYOMO

**Ukurasa**

**UTANGULIZI…………………………………………………….........................................…..**vi
Malengo ya Jumla ya Kufundisha Taaluma ya Kiswahili katika mafunzo ya ualimu................vii

Ujuzi wa Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti katika somo la Kiswahili…......................................................................................................................vii

Malengo ya kufundisha Kiswahili katika Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti……………………….....................................................................................................viii

Muundo wa muhtasari………………………………….....................................................viii

Muda wa Mafunzo………………………………………………………………….……..ix

Upimaji.................……………………………............………………………………………..x

Sehemu ya kwanza: Taaluma……….........................…...………………………….............1

Sehemu ya pili: Ufundishaji.......................................................................................................................20

## UTANGULIZI

Muhtasari huu wa 2009 ni toleo la Muhtasari wa Kiswahili Ualimu Ngazi ya Cheti uliohaririwa. Mambo mengi na mbinu za kufundishia na kujifunzia zimebadilika kwa kuzingatia maendeleo ya fikra, sayansi na teknolojia. Mada za muhtasari huu zinamwelekeza mkufunzi kuwa mbunifu na kuwafikirisha wanachuo wake.

Sababu za kuwa na muhtasari huu zimetokana na kuwapo kwa malengo mbalimbali ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Miongoni mwa malengo hayo ni kupata wataalam bora. Aidha dira ya elimu ni kuandaa walimu wenye taaluma bora. Mwelekeo wake ni kutoa walimu wenye ujuzi wa kufahamu na kupima maendeleo ya wanafunzi na kutatua matatizo yao katika kujifunza. Pia tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa walimu wa Kiswahili katika shule za Msingi wanahitaji kuimarishwa katika utaalamu wa kufundisha darasani na kwenye taaluma ya lugha ya Kiswahili. Hivyo muhtasari huu umeandaliwa ili kukidhi mahitaji ya utaalamu na kumwezesha mwalimu kulimudu vyema somo la Kiswahili.

Kozi ya somo la Kiswahili katika shule za msingi ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili. Muhtasari huu una sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ya taaluma na ya pili ni ya Ufundishaji. Katika sehemu ya kwanza mwanachuo atajifunza mada za kitaaluma na kupata ujuzi katika masuala ya lugha na fasihi. Katika sehemu ya pili mwanachuo atajifunza ufundishaji kwa kutumia mbinu anuai katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Masuala mtambuko na ya wanafunzi wenye mahitaji maalum yamechopekwa katika mbinu za kufundishia.

Mkufunzi na uongozi wa chuo wahakikishe kwamba muhtasari huu unatekelezwa na kukidhi haja za wanachuo wenye mahitaji maalum kama kutumia lugha ya alama na ishara kwa viziwi, herufi za vidutu (Breili) kwa wasioona na maandishi makubwa kwa wenye uoni hafifu.

Katika sehemu ya ufundishaji kumewekwa mada mbili teule kutoka kwenye muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi (2005) zilizopendekezwa kufundishwa. Mada hizo ni mashairi na ufahamu. Mkufunzi anashauriwa kuonesha wanachuo namna ya kufundisha mada hizo teule kwa wanafunzi wa shule za msingi. Wanachuo nao wanatarajiwa kufundisha mmoja mmoja kama mkufunzi au mwalimu alivyoonesha namna ya kufundisha. Mada hizi zimetokea kama mazoezi ya kufundisha utungaji wa mashairi na ufupisho. Hizi mada mbili zimeteuliwa kama mifano ya

kumsaidia mkufunzi na wanachuo. Ufafanuzi wa mada hizi unatarajiwa kumsaidia mkufunzi aibue ubunifu wake na kuchakata mada nyingine vivyo hivyo.

## MALENGO YA JUMLA YA KUFUNDISHA TAALUMA YA KISWAHILI KATIKA MAFUNZO YA UALIMU

Malengo ya jumla ya kufundisha Kiswahili katika vyuo vya ualimu ngazi ya cheti Tanzania yanatarajiwa kuwa:

a) Kuelewa kuwa Kiswahili ni sehemu ya utamaduni wa mtanzania.
b) Kuwa na tabia ya udadisi katika masuala ya lugha na fasihi ya Kiswahili.
c) Kujenga mwelekeo chanya katika kufundisha Kiswahili.
d) Kuelewa vipengele mbalimbali vya taaluma ya somo la Kiswahili.
e) Kujenga tabia ya kutumia Kiswahili fasaha katika Mawasiliano.
f) Kutumia Kiswahili kwa kuzingatia mwelekeo chanya kwenye masuala mtambuko na haki za binadamu.
g) Kutumia Kiswahili kuendeleza ujasiriamali.
h) Kuboresha welewa wa taaluma ya Kiswahili.

## UJUZI WA MAFUNZO YA UALIMU WA ELIMU YA SHULE YA MSINGI NGAZI YA CHETI KATIKA SOMO LA KISWAHILI.

Baada ya kozi hii mwalimu mwanafunzi anatarajiwa apate ujuzi ufuatao:-

a) kuandika na kuzungumza Kiswahili kwa usahihi kwa kuzingatia ubunifu na kufikiri kwa makini..
b) kupima maendeleo ya wanafunzi kitaaluma na kitabia.
c) kufundisha wanafunzi wa shule za msingi kwa kuzingatia ubunifu na tekinolojia za kisasa.
d) kubuni, kutengeneza na kutumia zana katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili.
e) kufanya tafiti ndogo ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.
f) kuboresha uwezo wake wa taaluma ya Kiswahili.

g) kuelekeza wanafunzi watunge kazi mbalimbali za kifasihi zinazoweza kuwaingizia kipato.

## MALENGO YA KUFUNDISHA KISWAHILI KATIKA UALIMU WA ELIMU YA MSINGI NGAZI YA CHETI

Baada ya mafunzo ya ualimu, mwalimu mwanafunzi aweze:

a) kutumia msamiati na miundo ya Kiswahili kwa usahihi katika maandishi na mazungumzo.
b) kutumia lafudhi ya Kiswahili kwa usahihi.
c) kufundisha somo la Kiswahili kwa njia shirikishi.
d) kutumia vifaa vyenye maudhui mbalimbali yakiwamo na masuala mtambuko na haki za binadamu katika kufundisha mada mbalimbali za Kiswahili.
e) kuboresha uelewa wake wa Kiswahili kitaaluma kwa kiwango cha kidato cha nne.
f) kuongoza wanafunzi watunge na waandike mashairi, hadithi na maigizo yanayoweza kuwaletea kipato.

### Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu una sehemu mbili. Sehemu ya kwanza yenye kurasa za awali inajumuisha: maelezo kuhusu muhtasari na sababu za kuboresha muhtasari, malengo ya jumla ya kufundisha taaluma ya Kiswahili katika mafunzo ya Ualimu, Ujuzi na Malengo ya kufundisha Kiswahili katika ualimu wa elimu ya msingi ngazi ya Cheti, muundo wa muhtasari, muda wa mafunzo na upimaji.

Sehemu ya pili inajumuisha sehemu ya Taaluma na Ufundishaji pamoja na mada zake teule. Muhtasari huu unazingatia mabadiliko na maendeleo katika utaalamu wa elimu. Unamdokeza mkufunzi mambo anayotakiwa ayazingatie. Muhtasari pia haumfungi mkufunzi kufikiri na kubuni mbinu na vifaa vya kutumia kufundishia. Kwa msingi huu mkufunzi anashauriwa kutumia mbinu na njia zilizopendekezwa katika muhtasari pamoja na mbinu na njia nyingine atakazoona zinafaa katika ujifinzaji na ufundishaji.

Muhtasari umeandikwa katika muundo wa maelezo yaliyotiririshwa (bila majedwali) kama ifuatavyo:-

a) Mada kuu
b) Mada ndogo
c) Malengo mahususi
d) Mbinu za kufundishia na kujifunzia
e) Zana za kufundishia na kujifunzia
f) Upimaji

Kila mada ndogo imejengwa kwa kutumia vipengele vifuatavyo:-

a) Muda unaopendekezwa kutumiwa katika kujifunza mada ndogo hiyo.
b) Malengo mahususi yanayotarajiwa kufikiwa katika kufundisha mada ndogo hiyo.
c) Mbinu za kufundishia na kujifunzia mada ndogo zimependekezwa. Inasisitizwa kwamba mkufunzi atumie mbinu zilizopendekezwa katika muhtasari pamoja na nyingine shirikishi atakazoona zinafaa.
d) Zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia pia zimependekezwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana na vifaa vilivyopendekezwa katika muhtasari pamoja na vingine atakavyoona vinafaa kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Muda wa Mafunzo**

Sehemu ya kwanza ya muhtasari huu ambayo ni ya Taaluma imekadiriwa kufundishwa kwa muda wa saa 128. Jumla hii inatokana na ukokotoaji ufuatao: Kila mwaka una miezi nane (8) ya mafunzo ya nadharia na miezi miwili (2) ya mafunzo ya vitendo. Muhula wa kwanza una wiki 20 za taaluma ambayo ikizidishwa kwa saa mbili (2) kwa wiki tunapata saa 40 kwa muhula. Muhula wa pili una wiki 12 za taaluma ambazo zikizidishwa kwa saa 2 kwa wiki tunapata saa 24 kwa muhula huo. Kwa hiyo saa za nadharia ni 64 kwa mwaka mmoja. Hii ni sawa na saa 128 kwa miaka miwili (2). Saa hizo zimesambazwa kwenye mada ndogo ndani ya maudhui ya sehemu ya kwanza ya muhtasari huu.

Sehemu ya pili ya muhtasari ambayo ni ya Ufundishaji imekadiriwa kufundishwa kwa saa 192. Ukokotoaji wake uko hivi: Kila mwaka una miezi nane (8) ya mafunzo ya nadharia na miwili (2)

ya mafunzo ya vitendo. Muhula wa kwanza una wiki 20 za taaluma ambayo ikizidishwa kwa saa tatu (3) kwa wiki tunapata saa 60 kwa muhula. Muhula wa pili una wiki 12 za taaluma ambazo zikizidishwa kwa saa 3 kwa wiki tunapata saa 36 kwa muhula huo. Kwa hiyo saa za nadharia ni 96 kwa mwaka mmoja. Hii ni sawa na saa 192 kwa miaka miwili (2). Saa hizo zimesambazwa kwenye mada ndogo ndani ya maudhui ya sehemu ya pili ya muhtasari huu.

Ni muhimu kuwahamasisha wanachuo kujenga tabia ya kujisomea katika maktaba na kwenye tovuti. Ni vizuri kutumia mazoezi ya kufanyia nyumbani na kazi mradi zitakazowashawishi kujisomea.

Jedwali lifuatalo linaonesha mtawanyo wa muda huo kwa mihula 2

| **Kiswahili** | **Mwaka wa kwanza**<br>**Muhula wa kwanza** | **Mwaka wa kwanza**<br>**Muhula wa pili** | **Mwaka wa pili**<br>**Muhula wa kwanza** | **Mwaka wa pili**<br>**Muhula wa pili** | **Jumla ya miaka miwili** |
|---|---|---|---|---|---|
| Taaluma | 40 | 24 | 40 | 24 | **128** |
| Ufundishaji | 60 | 36 | 60 | 36 | **192** |

**Upimaji**

Kumewekwa mapendekezo ya namna ya kuwapima wanachuo katika mada ndogo. Upimaji huo unatakiwa uwe endelezi. Huu ni upimaji unaozingatia uelewa na utendaji wa mwanachuo kabla ya, wakati wa na baada ya kujifunza mada kuu au mada ndogo fulani. Kwa ujumla, kuna aina mbili za upimaji.

Kwanza ni upimaji endelezi unaoongozwa na mkufunzi na kupewa uzito wa asilimia 50 ya alama zote. Upimaji huu unajumuisha vipengele vya: Taaluma, Ufundishaji, Mtihani wa mwisho wa muhula na Mazoezi ya kufundisha ya muda mfupi. Pili ni upimaji tamati unaofanywa na Baraza la Mitihani la Taifa na una uzito wa asilimia 50 ya alama zote.

Katika upimaji endelezi mwalimu anashauriwa kuwapima wanachuo kwa kutumia mbinu mbalimbali za upimaji ili kukuza uwezo wa wanafunzi kulimudu somo wakati wa ufundishaji na

ujifunzaji. Alama za upimaji endelezi zilizooneshwa katika jedwali la upimaji ni zile tu zitakazounganishwa na alama za upimaji tamati. Mkufunzi anashauriwa agawe alama kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hilo.

**Jedwali la Upimaji Endelezi na Tamati**

| | | **Mwaka 1** | | **Mwaka 2** | | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Upimaji endelezi | | **Muhula 1** | **Muhula 2** | **Muhula 1** | **Muhula 2** | |
| a) Taaluma | Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 05 |
| | Kazi Mradi | - | 1 | 1 | - | 05 |
| | Mitihani ya mihula | 1 | 1 | 1 | - | 10 |
| b)Ufundishaji | Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 05 |
| | Ufundishaji Muda mfupi | 1 | 1 | 1 | - | 05 |
| | Utungaji wa insha | 1 | 1 | - | - | 10 |
| | Mitihani ya Mihula | 1 | 1 | 1 | - | 10 |
| 2. Mitihani ya mwisho (BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA) | | | | | | 50 |
| **Jumla kuu** | | | | | | **100** |

## SEHEMU YA KWANZA: TAALUMA

### Ujuzi wa somo

Baada ya kozi ya miaka miwili mwanachuo awe na ujuzi wa:

a) Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali.

b) Kuwasiliana kwa Kiswahili katika shughuli za kila siku katika mazingira mbalimbali.

c) Kukipenda na kukithamini Kiswahili kama lugha ya Taifa na ya kimataifa.

d) Kujisomea maandiko ya kiada na ziada kwa ufahamu ili kupata maarifa na burudani.

e) Kutumia lugha ya Kiswahili katika kuendeleza masuala mtambuko.

f) Kuimarisha ujuzi wa kitaaluma wa mwanafunzi katika lugha ya Kiswahili.

g) Kujenga mtazamo chanya wa mwanafunzi kwenye lugha ya Kiswahili.

h) Kujenga tabia za udadisi na ubunifu katika masuala ya lugha ya Kiswahili.

### Malengo ya somo:

Baada ya kozi ya miaka miwili mwanachuo aweze:

a) Kutumia Kiswahili fasaha katika hali na miktadha mbalimbali katika kusikiliza,

b) kuzungumza, kusoma na kuandika.

c) Kutumia Kiswahili kupata maarifa, stadi na mienendo ya kijamii, kiutamaduni, kiteki- nolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.

d) Kutumia lugha ya kisanii katika miktadha mbalimbali.

e) Kuthamini Kiswahili kama sehemu muhimu ya utamaduni wa mtanzania.

f) Kuendeleza tabia ya udadisi na ubunifu katika masuala ya lugha na fasihi ya Kiswahili

g) Kutambua jinsi lugha inavyoweza kushughulikia masuala mtambuko.

h) Kuimarisha uelewa wake wa Kiswahili kitaaluma.

## 1.0 STADI ZA LUGHA

### 1.1 Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza.

**Muda: Saa 8**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhima za stadi ya kusikiliza na kuzungumza.

b) Kueleza uhusiano uliopo kati ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza

c) Kuzungumza kwa ufasaha.

d) Kueleza jinsi ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Onesho mbinu, igizo, dhima, bungua bongo, maswali na majibu ili kufafanua stadi ya kusikiliza na kuzungumza.

b) Kujadili katika vikundi dhima za stadi ya kusikiliza na kuzungumza na kueleza uhusiano uliopo kati ya stadi hizo.

c) Majadiliano ya pamoja kuhusu dhima za stadi za kusikiliza na kuzungumza na kueleza uhusiano wake.

d) Mazoezi ya kusikiliza na kuzungumza kwa mwanachuo mmoja mmoja na kurekebisha makosa ya kimatamshi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Kanda zenye taarifa za matukio mbalimbali yaliyorekodiwa katika mazingira halisi.

**Upimaji**

a) Majaribio ya kupima uelewa wa mwanachuo kuhusu dhima za stadi ya kusikiliza na kuzungumza na uhusiano uliopo kati ya stadi hizo.

b) Maswali na majibu kupima uelewa wa mwanachuo kuhusu kuzungumza kwa ufasaha.

c) Fomu ya mlinganisho wa viwango vya stadi ya kusikiliza kwa makini na ufasaha wa kuzungumza.

## 1.2 Stadi ya Kusoma

**Muda: Saa 9**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhima za stadi ya kusoma.
b) Kujadili sababu zinazomfanya mwanafunzi kushindwa kusoma.
c) Kusoma kwa usahihi.
d) Kueleza jinsi ya kufundisha kusoma.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi kufafanua dhima za stadi ya kusoma na sababu zinazomfanya mwanafunzi kushindwa kusoma.
b) Majadiliano ya pamoja kufafanua dhima za stadi ya kusoma.
c) Maswali na majibu, kutaja mambo ya kuzingatia katika kusoma kwa usahihi.

d) Mwanachuo mmoja mmoja kusoma kwa usahihi matini mbalimbali zikiwemo zenye kujibu maswali kutokana na matini walizosisoma.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini mbalimbali zikiwemo zenye masuala mtambuko kama elimu ya UKIMWI na usawa wa jinsia.

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa wa mwanachuo.

b) Mazoezi ya kusoma kwa kuzingatia matamshi sahihi na matumizi ya vituo.

c) Mazoezi ya kujibu maswali ya ufahamu.

## 1.3 Stadi ya Kuandika

**Muda: Saa 9**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua dhima za stadi ya kuandika.
b) Kufafanua fasili na dhima za imla.
c) Kuandika imla
d) Kueleza jinsi ya kufundisha kuandika imla.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji, kufafanua dhima za stadi ya kuandika, dhima za imla na mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika imla.

b) Kusoma katika maktaba na kuainisha stadi za kuandika.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini kwa ajili ya kusoma imla

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio kupima uelewa wa stadi ya kuandika.
b) Kuandika imla.

## 2.0 UTUNGAJI

### 2.1 Insha

**Muda: Saa 11**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili na dhima za insha.
b) Kuainisha aina mbili za insha.
c) Kuandika insha mbalimbali

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu, majadiliano ya vikundi na uwasilishaji kueleza fasili na dhima za insha na aina ya insha.

b) Mwanachuo mmoja mmoja aandike insha.

c) Kazi mradi ya kuandika insha mbalimbali zikiwemo zenye maudhui ya elimu ya mazingira, usawa wa jinsia, rushwa, madawa ya kulevya na ajira ya mtoto.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati ya muundo wa insha na insha za mifano.

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kupima uwezo wa mwanachuo katika kueleza fasili na dhima za insha, kuainisha aina za insha, na kupima ujuzi wa mwanachuo wa kuandika insha.

## 2.2 Barua

**Muda: Saa 8**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhima za barua.
b) Kujadili muundo wa barua za kirafiki na rasmi.
c) Kuandika barua ya kirafiki na rasmi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji kueleza dhima za barua na wajadili muundo wa barua za kirafiki na rasmi.

b) Majadiliano ya pamoja juu ya muundo wa barua za kirafiki na barua rasmi kuongoza majadiliano ya pamoja.

c) Utafiti juu ya aina mbalimbali za barua.

d) Mwanachuo mmoja mmoja aandike barua ya kirafiki na rasmi

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati ya muundo wa barua za kirafiki na rasmi na barua za mifano.

**Upimaji**

a) Mazoezi kupima uelewa wa wanachuo.
b) Mazoezi ya uandishi wa barua za kirafiki na rasmi.

**Simu ya Maandishi**

**2.3 Muda: Saa 4**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kujadili muundo wa simu ya maandishi.
b) Kueleza umuhimu wa simu ya maandishi.
c) Kuandika simu ya maandishi kutokana na vifungu vya habari.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano muundo wa simu ya maandishi.
b) Maswali na majibu na majadiliano ya vikundi kueleza umuhimu wa simu ya maandishi.
c) Majadiliano ya pamoja kuhusu umuhimu na muundo wa simu ya maandishi
d) Mwanachuo mmoja mmoja aandike simu ya maandishi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Simu ya maandishi ya mfano:

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kupima uelewa wa mwanachuo.

b) Mazoezi ya kuandika simu ya maandishi.

## 2.4 Mashairi, Ngonjera na Tenzi

**Muda: Saa 8**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili na dhima za mashairi, ngonjera na tenzi.
b) Kuchanganua mashairi, ngonjera na tenzi.
c) Kutunga mashairi, ngonjera na tenzi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu, majadiliano ya vikundi, igizo dhima na nyimbo, fasili na dhima za mashairi, ngonjera na tenzi.
b) Wanafunzi katika jozi kuchanganua mashairi, ngonjera na tenzi.
   c) Katika vikundi wanachuo watunge mashairi na ngonjera.
   d) Kwa njia ya maonyesho vikundi viwasilishe mashairi waliyoyatunga.
   e) Maigizo kuwasilisha ngonjera zilizotungwa.
   f) Kwa njia ya kazi mradi wanachuo watunge tenzi mbalimbali.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini za mashairi, ngonjera na tenzi zikiwemo zenye ujumbe wa ufisadi, kujali wenye ulemavu, rushwa, mimba katika umri mdogo, madawa ya kulevya na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kupima uelewa wa wanachuo.
b) Mazoezi ya kutunga mashairi, ngonjera na tenzi.

## 3.0 FASIHI SIMULIZI

### 3.1 Fasili ya Fasihi Simulizi

**Muda: Saa 8**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza fasili ya fasihi simulizi.

b) Kufafanua tanzu za fasihi simulizi.

c) Kujadili dhima za fasihi simulizi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kwa njia ya bungua bongo na maswali na majibu wanachuo waeleze fasili ya fasihi simulizi.

b) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji kufafanua tanzu na dhima za fasihi simulizi.

c) Kusikiliza matini za fasihi simulizi zilizorekodiwa na kujibu maswali yanayohusiana na matini hizo. Mkufunzi aongoze majadiliano ya pamoja.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Matini zenye kazi za fasihi simulizi kama mashairi, ngonjera, hadithi na nyimbo.

b) Kanda zilizorekodiwa kazi za fasihi simulizi kama maigizo, ngonjera, nyimbo na hadithi.

**Upimaji**

Mazoezi, utafiti na majaribio ya kupima uelewa wa wanachuo kuhusu fasili, tanzu na dhima za fasihi simulizi.

## 3.2 Methali

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili na dhima za methali.
b) Kukusanya methali mbalimbali.
c) Kutumia methali katika miktadha inayofaa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi, maswali na majibu na uwasilishaji kueleza fasili na dhima za methali.

b) Majadiliano ya pamoja kuboresha kazi walizowasilisha.

c) Kazi mradi kukusanya methali mbalimbali za lugha ya Kiswahili.

d) Matembezi ya galari kuwasilisha methali mbalimbali za Kiswahili.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati yenye methali mbalimbali.

**Upimaji**

Majaribio kupima uelewa na matumzi ya fasili, dhima na methali katika miktadha anuai.

## 3.3 Nahau

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili na dhima za nahau
b) Kukusanya nahau mbalimbali shuleni na kwenye ujirani wa shule.
c) Kutumia nahau katika miktadha inayofaa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu na majadiliano ya vikundi kueleza fasili ya fasihi, dhima na matumizi ya nahau.
b) Wanachuo wawasilishe kazi zao kwa vikundi
c) Majadiliano ya pamoja kuboresha kazi zao.
d) Kazi mradi kukusanya nahau mbalimbali.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati ya nahau.
b) Vitu halisi

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa wa wanachuo.

## 3.4 Vitendawili.

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili ya Vitendawili.
b) Kujadili dhima za Vitendawili katika maisha ya kila siku.
c) Kutega na kutegua vitendawili.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu, chemsha bongo na majadiliano ya vikundi kueleza fasili na dhima za vitendawili.

b) Majadiliano ya pamoja ili wanachuo waweze kuboresha kazi zao.

c) Kazi mradi kukusanya vitendawili mbalimbali na kuviwasilisha darasani.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati ya vitendawili.

b) Vitu halisi

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa kuhusu fasili na dhima za vitendawili.
b) Zoezi kutega na kutegua vitendawili.

### 3.5 Hadithi

**Muda: Saa 6**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili ya hadithi.
b) Kujadili dhima za hadithi.
c) Kusimulia hadithi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu na chemsha bongo kueleza fasili ya hadithi.
b) Vikundi kuwasilisha kwa ajili ya majadiliano ya pamoja.
c) Wanachuo kusimulia hadithi na kisha kubainisha ujumbe uliomo kwenye kila hadithi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Picha zenye vitendo vinavyounda hadithi.
b) Matini zenye hadithi mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa kuhusu fasili na dhima ya hadithi.
b) Mazoezi ya kupima uwezo wa kusimulia hadithi.

## 4.0 UFAHAMU

### 4.1 Ufahamu wa Kusikiliza na Kusoma

**Muda: Saa 6**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza fasili ya ufahamu.
b) Kufafanua ufahamu wa kusikiliza na kusoma.
c) Kujadili dhima za ufahamu.
d) Kujibu maswali ya ufahamu.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo, maswali na majibu.
b) Vikundi vya majadiliano kufafanua ufahamu wa kusikiliza na kusoma dhima za ufahamu.
c) Uwasilishaji na majadiliano ya pamoja.
d) Mazoezi ya kusiliza kanda zenye matini zilizorekodiwa.
e) Kusoma matini zenye maudhui ya ajira ya mtoto, masuala ya mazingira, VVU/UKIMWI kisha wajibu maswali ya ufahamu.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kanda zenye matini zilizorekodiwa.
b) Matini zenye maudhui ya ajira ya mtoto, masuala ya mazingira, VVU/Ukimwi.

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa kuhusu fasili, dhima na ufahamu wa kusikiliza na kusoma.

## 4.2 Msamiati na Miundo.

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua maana ya msamiati

b) Kujadili umuhimu wa kufundisha msamiati na miundo.

c) Kuainisha mbinu za kutambua misamiati mbalimbali.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu kufafanua maana ya msamiati.

b) Majadiliano ya vikundi kuainisha mbinu za kutambua misamiati na umuhimu wa kufundisha msamiati na miundo.

c) Wanachuo wawasilishe kazi zao kwa vikundi.

d) Majadiliano ya pamoja kuhusu matini mbalimbali zenye msamiati na miundo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini mbalimbali zenye msamiati na miundo.

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa juu ya umuhimu wa kufundisha msamiati na miundo.

## 4.3 Kusoma Kimya.

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhima za kusoma kimya.
b) Kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma.
c) Kufupisha habari aliyoisoma kwa kiwango cha theluthi moja ya habari ya awali bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mtunzi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi na maswali na majibu kueleza dhima za kusoma kimya.
b) Wanachuo wasome habari kimya. Kisha wajibu maswali.
c) Katika vikundi wanachuo wafanye mazoezi ya kufupisha habari waliyoisoma bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mtunzi.
d) Vikundi kuwasilisha kazi zake ikifuatiwa na majadiliano ya pamoja.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini mbalimbali zikiwemo zenye masuala mtambuko.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kuandika, kuzungumza na majaribio ya kupima uelewa juu ya dhima za kusoma kimya.

b) Mazoezi ya kupima uwezo wa kufupisha habari.

## 4.4 Kusoma kwa Sauti

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kujadili dhima za kusoma kwa sauti
b) Kusoma kwa sauti, kwa kuzingatia matamshi, lafudhi sahihi na alama za usomaji.
c) Kujibu maswali kutokana na matini aliyoisoma

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji kuhusu dhima ya kusoma kwa sauti.

b) Mazoezi ya kusoma matini mbalimbali kwa sauti, mmoja mmoja kwa kuzingatia lafudhi sahihi na kuzingatia taratibu za uandishi.

c) Maswali na majibu kutokana na matini walizozisoma.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini zenye maudhui yanayohusu watoto wenye mahitaji maalum, rushwa, madawa ya kulevya na haki za binadamu.

**Upimaji**

a) Majaribio na mazoezi ya kupima uelewa juu ya dhima za kusoma kwa sauti.

b) Mazoezi na majaribio ya kupima uwezo wa kusoma kwa sauti kwa kuzingatia alama za vituo kwa matamshi sahihi.

## 5.0 SARUFI

### 5.1 Aina za Maneno

**Muda: Saa 3**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha aina za maneno katika sentensi za Kiswahili
b) Kufafanua kila aina ya neno
c) Kutumia aina za maneno kwa usahihi katika miktadha mbalimbali.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo maswali na majibu kubainisha aina za maneno katika sentensi za Kiswahili.

b) Vikundi vya majadiliano kuhusu aina za maneno katika lugha ya Kiswahili.

c) Kwa kutumia mti wa aina za maneno kuendesha majadiliano ya pamoja.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati inayoonyesha aina za maneno

**Upimaji**

a) Maswali na majibu na mazoezi kupima uelewa kuhusu ubainishaji wa aina za maneno katika sentensi za Kiswahili.

b) Mazoezi kupima uwezo wa kutumia aina za maneno kwa usahihi katika miktadha mbalimbali.

## 5.2 Kauli za Utendaji

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya kauli za utendaji

b) Kubainisha kauli za utendaji

c) Kutumia kauli za utendaji katika miktadha mbalimbali

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu kueleza maana ya kauli za utendaji.

b) Vikundi vya majadilaino kubainisha kauli mbalimbali za utendaji.

c) Uwasilishaji wa vikundi ikifuatiwa na majadiliano ya pamoja kwa kutumia chati ya kauli mbalimbali za utendaji.

d) Mazoezi ya kutunga sentensi mbalimbali zenye kauli za utendaji.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati inayoonesha kauli mbalimbali za utendaji.

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kuzungumza, kuandika na kupima uelewa wa wanachuo kuhusu kauli za utendaji.

## 5.3 Kauli Halisi na Kauli Taarifa

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya kauli halisi na kauli taarifa.

a) Kubainisha kauli halisi na kauli taarifa.
b) Kutumia kauli halisi na kauli taarifa katika miktadha mbalimbali.

**Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia**

a) Bungua bongo, maswali na majibu katika kueleza maana ya kauli halisi na kauli taarifa.

b) Majadiliano ya vikundi kubainisha kauli halisi na kauli taarifa.

c) Uwasilishaji kubainisha kauli halisi na kauli taarifa ikifuatiwa na majadiliano ya pamoja.

d) Mwanachuo mmoja mmoja atunge sentensi mbalimbali za kauli halisi na kauli taarifa.

e) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji kubadili kauli halisi kuwa kauli taarifa.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini zenye kauli halisi na kauli taarifa

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kuzungumza, kuandika na kupima uwezo wa kueleza, kubainisha na kutumia kauli halisi na kauli taarifa.

**SEHEMU YA PILI: UFUNDISHAJI**

**Ujuzi wa Somo**

a) Baada ya kozi ya miaka miwili mwanachuo awe na ujuzi wa:

b) Kufundisha kwa njia shirikishi mada mbalimbali za somo la Kiswahili kwa Shule za Msingi.

c) Kutambua na kutatua matatizo mbalimbali ya wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

d) Kutengeneza, kufaragua na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kwa kuzingatia mahitaji mbalimbali ya wanafunzi

e) Kuwasaidia na kujali wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Malengo ya Somo:**

Baada ya kozi ya miaka miwili mwanachuo aweze:

a) Kutumia mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunzia mada zote za muhtasari wa Kiswahili katika shule za msingi.

b) Kutengeneza, kufaragua na kutumia zana anuai za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

c) Kutumia matini zenye masuala mtambuko katika kufundishia mada mbalimbali za somo la Kiswahili.

d) Kutambua matatizo mbalimbali ya wanafunzi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

e) Kufundisha stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi pamoja na wenye mahitaji maalumu.

## 1.0 MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA KISWAHILI

### 1.1 Misingi ya kufundishia na kujifunzia Kiswahili

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili

b) Kufafanua misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili

c) Kutumia misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili katika ufundishaji wa somo la Kiswahili

**Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia**

a) Maswali na majibu kutaja misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

b) Vikundi vya majadiliano na uwasilishaji kufafanua misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

c) Kwa kutumia chati ya stadi za lugha, kuongoza majadiliano ya pamoja na mhadhara mfupi kufafanua misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

d) Onesha mbinu kuhusu misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili katika ufundishaji wa mada zilizomo katika muhtasari wa Kiswahili shule za msingi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati ya stadi za lugha

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa wa kueleza na kutumia misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

## 1.2 Mbinu Anuai za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili.

**Muda: Saa 21**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kutaja mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.
b) Kujadili mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.
c) Kueleza ubora na upungufu wa mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu katika majadiliano ya vikundi kuhusu mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.
b) Kuwasilisha kazi kwa vikundi ikifuatiwa na majadiliano ya pamoja.
c) Kwa kutumia mchoro wa mti unaoonesha mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kuongoza majadiliano ya pamoja.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Mchoro wa mti unaoonesha mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa kuhusu mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

b) Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa kuhusu ubora na upungufu wa mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

## 2.0 UCHAMBUZI WA VIFAA VYA MTAALA WA KISWAHILI

### 2.1 Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili.

**Muda: Saa 21**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutaja vifaa vya mtaala wa somo la Kiswahili.
b) Kufafanua vifaa vya mtaala wa somo la Kiswahili.
c) Kuchambua sifa za kila kifaa.

**Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia**

a) Maswali na majibu na bungua bongo.
b) Majadiliano ya vikundi kufafanua na kuchambua sifa za vifaa vya mtaala wa somo la Kiswahili.
c) Uwasilishaji wa kazi za vikundi.

d) Kwa kutumia muhtasari wa somo la Kiswahili, vitabu vya kiada na ziada na kiongozi cha mwalimu, kufanya majadiliano ya pamoja.
e) Mhadhara mfupi kuhusu uchambuzi wa vifaa vya mtaala wa somo la Kiswahili.

**Zana/Vifaa vya Kufundisha**

Muhtasari, vitabu vya kiada, vitabu vya ziada, kiongozi cha mwalimu n.k.

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio ya kupima uelewa kuhusu vifaa vya mtaala wa somo la Kiswahili.

## 3.0 MAANDALIZI YA KUFUNDISHA SOMO LA KISWAHILI

### 3.1 Uchambuzi wa Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Shule za Msingi.

**Muda: Saa 18**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutathmini utoshelevu wa utangulizi na malengo ya muhtasari.
b) Kubainisha mada mbalimbali za muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi.
c) Kuhakiki ubora wa maudhui na mpangilio wa mada katika muhtasari wa Kiswahili kwa shule za msingi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Wanachuo wakae katika vikundi.

   i) Watathmini utangulizi na malengo ya muhtasari.

   ii) Wabainishe mada mbalimbali za muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi.

   iii) Wahakiki ubora wa maudhui na mpangilio wa mada katika muhtasari wa Kiswahili kwa shule za msingi.

b) Kila kikundi kiwasilishe kazi zake.

c) Kwa kutumia muhtasari wa Kiswahili kwa shule za msingi kuongoza majadiliano ya pamoja. Kisha wanachuo waboreshe kazi zao.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Muhtasari wa Kiswahili kwa shule za msingi.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kupima uelewa kuhusu ubora wa maudhui na mpangilio wa mada katika muhtasari wa Kiswahili kwa shule za msingi.

b) Vitendo vya kupima uwezo wa kubaini mada mbalimbali za Muhtasari wa Kiswahili kwa shule za Msingi.

## 3.2 Azimio la Kazi

**Muda: Saa 18**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha vipengele vya azimio la kazi.
b) Kubainisha vipengele vya muhtasari vinavyotakiwa kuingia katika azimio la kazi.
c) Kutayarisha azimio la kazi.
d) Kujadili faida za azimio la kazi

**Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia**

a) Maswali na majibu na bungua bongo kubainisha vipengele vya azimio la kazi na vipengele vya muhtasari vinavyotakiwa kuingia katika azimio la kazi.

b) Kutayarisha azimio la kazi kwa vikundi.

c) Majadiliano ya vikundi kuhusu faida za kuandaa azimio la kazi na kisha kufanya uwasilishaji

d) Kila kikundi kiwasilishe kazi zake.

e) Kwa kutumia muhtasari wa Kiswahili kwa shule za msingi na azimio la kazi kuongoza majadiliano ya pamoja.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Muhtasari, vitabu vya kiada na kalenda ya shule.

b) Azimio la kazi la mfano.

**Upimaji**

a) Zoezi la kubainisha vipengele vya azimio la kazi.

b) Zoezi na majaribio ya kuandaa azimio la kazi.

c) Mkoba wa kazi juu ya maazimio ya kazi ya somo la Kiswahili

## 3.3 Andalio la Somo.

**Muda: saa 18**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha vipengele vya andalio la somo.
b) Kubainisha maudhui ya azimio la kazi yanayotakiwa kuingia katika andalio la somo.
c) Kutayarisha andalio la somo.
d) Kujadili faida za andalio la somo.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu na bungua bongo kubainisha vipengele vya andalio la somo na vipengele vya azimio la kazi vinavyotakiwa kuingia katika andalio la somo.

b) Katika vikundi kuandaa andalio la somo kwa kutumia azimio la kazi na kueleza faida za kuandaa andalio la somo.

c) Uwasilishaji na majadiliano ya pamoja na kuboresha kazi zao.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Andalio la somo la mfano.

b) Azimio la kazi, vitabu vya kiada, ziada na rejea.

**Upimaji**

a) Zoezi na majaribio ya kupima uelewa wa kubainisha vipengele vya andalio la somo.

b) Zoezi la kuandaa andalio la somo.

c) Mkoba wa kazi juu ya maandalio ya somo la Kiswahili.

## 3.4 Shajara ya Somo

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua vipengele vya shajara ya somo.

b) Kubainisha maudhui ya azimio la kazi yanayotakiwa kuingia katika shajara ya somo.

c) Kuandaa na kutumia shajara ya somo.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Mhadhara mfupi kufafanua vipengele vya shajara ya somo na kubainisha maudhui ya azimio la kazi yanayotakiwa kuingia katika shajara ya somo.

b) Majadiliano ya vikundi kuhusu umuhimu wa kuandaa shajara ya somo

c) Uwasilishaji kwa njia ya matembezi ya galari.

d) Kwa kutumia azimio la kazi na shajara ya somo na mfano kuongoza majadiliano ya pamoja. Kisha wanachuo waboreshe kazi zao.

e) Mwanachuo mmoja mmoja aandae shajara ya somo na kisha kuwasilisha kwa njia ya maonyesho.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Shajara ya somo ya mfano.

b) Azimio la kazi.

**Upimaji**

a) Zoezi la kuandaa shajara ya somo na kuitumia.

b) Mkoba wa kazi juu ya shajara la somo la Kiswahili.

## 3.5 Mazoezi ya Ufundishaji: Utungaji wa Mashairi

**Muda: Saa 15**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kujadili mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa mashairi.
b) Kutunga mashairi akizingatia urari wa vina na mizani.
c) Kufundisha jinsi ya kutunga mashairi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa mashairi. Kisha vikundi kuwasilisha kwa ajili ya majadiliano ya pamoja.
b) Mwanachuo mmoja mmoja atunge shairi akizingatia urari wa vina na mizani na kisha kuwasilisha katika vikundi vya majadiliano.
c) Mhadhara mfupi kujadili jinsi ya kufundisha utungaji wa mashairi.

d) Onesho mbinu jinsi ya kufundisha mada ya utungaji wa mashairi kwa wanafunzi wa darasa la saba.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini mbalimbali za mashairi zikiwemo zenye maudhui ya masuala mtambuko.

**Upimaji**

a) Zoezi la kupima uelewa kuhusu mambo ya kuzingatia katika utungaji wa mashairi.

b) Mazoezi na mkoba wa kazi ili kupima utungaji wa mashairi kwa kuzingatia urari wa vina na mizani.

c) Mazoezi ya kupima uwezo wa kufundisha utungaji wa mashairi.

## 3.6 Mazoezi ya Ufundishaji: Ufupisho

**Muda: Saa 8**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma.
b) Kusimulia habari aliyoisoma kwa maneno yake mwenyewe.
c) Kufupisha habari hadi theluthi moja ya habari ya awali.
d) Kufundisha ufupisho kwa kutumia mbinu shirikishi na zana zinazofaa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kusoma kimya kifungu cha habari. Kisha wajibu maswali kutokana na habari waliyoisoma.

b) Mwanachuo mmoja mmoja asimulie habari aliyoisoma kwa maneno yake mwenyewe bila kupoteza maana ya awali ya habari hiyo.

c) Majadiliano ya pamoja jinsi ya kufupisha habari hadi theluthi moja ya habari ya awali waliyoisoma.
d) Mwanachuo mmoja mmoja afupishe habari hadi theluthi moja ya habari ya awali.
e) Mhadhara mfupi jinsi ya kufundisha ufupisho kwa wanafunzi wa shule za msingi.
f) Onesho mbinu jinsi ya kufundisha ufupisho kwa wanafunzi wa darasa la tano.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Matini za ufahamu zenye maudhui ya ajira ya mtoto, elimu ya ukimwi, elimu ya mazingira, usalama barabarani na watoto wenye mahitaji maalumu.

**Upimaji**

a) Zoezi na majaribio kupima uwezo wa kujibu maswali, kusimulia habari aliyoisoma/sikia na kufupisha habari.

b) Mazoezi ya kufundisha.

## 4.0 ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA

### 4.1 Utayarishaji wa Zana

**Muda: Saa 10**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua maana na umuhimu wa kutumia zana za kufundishia
b) Kueleza sifa za zana za kufundishia.
c) Kukusanya zana za kufundishia somo la Kiswahili kulingana na mada husika.
d) Kutengeneza zana za kufundishia kulingana na vitu vilivyomo kwenye mazingira kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi.
e) Kufaragua zana za kufundishia kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vikundi vya majadiliano kufafanua maana na umuhimu wa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.
b) Uwasilishaji na majadiliano ya pamoja.
c) Maswali na majibu kueleza sifa za zana za kufundishia.
d) Kazi mradi kukusanya zana za kufundishia somo la Kiswahili kulingana na mada husika.
e) Mazoezi ya vitendo kutengeneza zana za kufundishia kulingana na mazingira kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi na kisha kuwasilisha kwa njia ya matembezi ya galari.
f) Onesho mbinu kuonyesha ufaraguaji wa zana za kufundishia na kujifunzia.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Chati, kadi za maneno, michoro na vitu halisi.

**Upimaji**

a) Zoezi la kupima uelewa kuhusu sifa, maana na umuhimu wa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.
b) Kazi mradi kukusanya na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.

## 4.2 Matumizi ya Zana

**Muda: Saa 6**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza namna ya kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji.
b) Kutumia zana mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi kuhusui matumizi ya zana katika ufundishaji na ujifunzaji.
b) Uwasilishaji na majadiliano ya pamoja.
c) Onesho mbinu kufundisha na kutumia zana za ufundishaji na ujifunzaji.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.**

Vifaa mbalimbali vilivyotengenezwa au kukusanywa na wanachuo.

**Upimaji**

Zoezi la kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 5.0 UPIMAJI

### 5.1 Majazi ya Elimu

**Muda: Saa 15**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha ngazi anuai za majazi ya elimu.
b) Kueleza matumizi ya ngazi za majazi ya elimu.
c) Kuandaa jedwali la kutahinia la mfano.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi kubainisha ngazi anuai za majazi ya elimu na matumizi ya ngazi hizo.
b) Uwasilishaji na majadiliano ya pamoja.
c) Kwa kutumia chati ya majazi ya elimu kuongoza majadiliano ya pamoja.
d) Kwa kutumia jedwali la kutahini, wanachuo katika vikundi kuandaa jedwali la kutahinia la mfano na kisha kuwasilisha kwa njia ya maonyesho.
e) Mwanachuo mmoja mmoja aandae jedwali la mfano la kutahinia na awasilishe kwa njia ya matembezi ya galari.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati ya jedwali la kutahinia.

b) Jedwali la kutahinia la mfano.

c) Chati ya majazi ya elimu.

**Upimaji**

b) Mazoezi ya kuandaa jedwali la kutahinia.

c) Mkoba wa kazi kuhusu jedwali la kutahinia.

## 5.2 Kutunga na Kusahihisha Maswali ya Zoezi, Jaribio na Mtihani.

**Muda: Saa 15**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kujadili aina mbalimbali za maswali.
b) Kutunga maswali ya aina mbalimbali kwa kuzingatia jedwali la kutahinia.
c) Kuandaa mwongozo wa kusahihishia.
d) Kutumia mwongozo wa kusahihishia mazoezi, majaribio na mitihani.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

(1) Majadiliano ya vikundi jinsi ya kutunga aina mbalimbali za maswali.

(2) Uwasilishaji na majadiliano ya pamoja jinsi ya kutunga aina mbalimbali za maswali.

(3) Majadiliano ya vikundi kuhusu jinsi ya kuandaa mwongozo wa kusahihishia.

(4) Kutunga maswali na kuandaa mwongozo wa kusahihishia katika vikundi na kisha kuwasilisha.

(5) Mhadhara mfupi na majadiliano ya pamoja kuboresha maswali na mwongozo wa kusahihishia maswali yaliyoandaliwa.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Matini yenye aina mbalimbali za maswali ya mitihani.

b) Mwongozo wa kusahihishia wa mfano.

c) Jedwali la kutahinia.

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio ya kuandaa aina mbalimbali za maswali ya mitihani.

b) Mkoba wa kazi kuhusu maswali mbalimbali ya mtihani na mwongozo wa usahihishaji.

**5.3 Matumizi ya alama za Mazoezi, Majaribio na Mitihani.**

**Muda: Saa 6**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutofautisha kati ya alama za mazoezi, majaribio na mitihani.

b) Kueleza matumizi mbalimbali ya alama za mazoezi, majaribio na mitihani.

c) Kutumia alama walizopata wanafunzi kuboresha ufundishaji.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu kutofautisha kati ya alama za mazoezi, majaribio na mitihani.

b) Kujadili katika vikundi kuhusu matumizi mbalimbali ya alama za mazoezi, majaribio na mitihani na jinsi ya kuzitumia ili kuboresha ufundishaji na kisha kuwasilisha kwa majadiliano ya pamoja.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Alama za mazoezi, majaribio na mitihani ya wanafunzi.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kutumia alama za mazoezi, majaribio na mitihani walizopata wanafunzi kuboresha ufundishaji.

## 6.0 UFUNDISHAJI WA MADA TEULE ZA SOMO LA KISWAHILI

### 6.1 Ufundishaji wa kukanusha matukio kwa "wakati ujao"

**Lengo Mahususi**

**Muda: Saa 10**

Baada ya kufundisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) kuandaa somo kwa dakika 20 la kukanusha matukio katika "wakati ujao"

b) kufundisha somo la wakati ujao kwa kutumia ufundishaji kiduchu

c) kutathmini somo na kutoa mwitiko

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Majadiliano katika jozi na uwasilishaji

b) Mazoezi ya darasani

c) Maswali na majibu

d) Igizo dhima

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Picha za matukio mbalimbali

b) Kalenda

c) Jedwali la matukio

**Mbinu za Upimaji**

a) Mazoezi darasani

b) Majaribio

c) Maswali na majibu

## 6.2 Ufundishaji wa kukanusha matukio ya "wakati uliopita"

**Muda: Saa 10**

**Lengo Mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) kuandaa somo la dakika 40 la kukanusha matukio kwa "wakati uliopita"

b) kufundisha somo katika shule iliyo jirani "Single Lesson Teaching Practice"

c) kutathmini na kutoa mwitiko wa somo

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo

b) Uwasilishaji wa majibu ya majadiliano

c) Majibu na maswali

d) Majadiliano ya vikundi

**Vifaa/Zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Picha za matukio mbalimbali

b) Chati ya ukutani ya sentensi za wakati uliopita

c) Kalenda

**Mbinu za upimaji**

a) Majaribio

b) Kazi za vikundi na uwasilishaji wake

c) Maswali na majibu

## 6.3 Ufundishaji wa kukanusha matukio kwa "wakati wa mazoea"

**Muda: Saa 11**

**Lengo mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) kuandaa somo la kukanusha matukio kwa wakati wa mazoea

b) kufundisha kwa kutumia ufundishaji wa mfano

c) kutathmini na kutoa mwitiko wa somo

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Majadiliano katika jozi

b) Igizo dhima

c) Maswali na majibu

d) Kusimulia hadithi

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Picha za matukio mbalimbali

b) Vitabu mbalimbali

c) Chati ya wakati wa mazoea

**Mbinu ya upimaji**

a) Maswali na majibu

b) Mazoezi darasani

c) Kazi za vikundi

d) Majaribio

## R E J E A


Taasisi ya Elimu Tanzania (2004**), *Moduli ya Somo la Mbinu za Kujifundishia Kiswahili, Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Chet*i.**

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003), ***Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu, Ngazi ya Cheti, Mbinu za Kufundishia Kiswahili.***

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2005), ***Muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi*.**